TANGAZO LA SERIKALI NA. 887 la tarehe 1/11/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1)*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA ZEPISA 'A' YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa katika Eneo la Zepisa 'A' ya Mwaka, 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji naMkurugenzi wa Jiji Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

MIPAKA YA ENEO ENEO LA URASIMISHAJI

"“Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ZPA1 yenye majira - nukta 823466.52MS, 9342617.16KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS53$^0$MS kwa umbali wa kilomita 2.48 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ZPA2 yenye majira - nukta 825471.60MS, 9341157.57KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa KS36$^0$MS kwa umbali wa kilomita 0.388 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ZPA3 yenye majira -

nukta 825238.89MS, 9340847.11KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KS78$^0$MG kwa umbali wa kilomita 2.266 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ZPA4 yenye majira - nukta 823022.50MS, 9341317.95KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa KS18$^0$'MS kwa umbali wa kilomita 1.373 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
28 Oktoba, 2024

DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*